**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA**
**SHULE YA SEKONDARI NYAMUNGA**

**S.L.P 1295**
**MUSOMA**
**09.11.2023**
**MOBILE: 0767 989 595**

**Kumb Na NSS/JOINT/VOL -1/2024**
**Jina la Mwanafunzi__________________________**
**S.L.P______________**

**Y AH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYAMUNGA KIDATO CHA KWANZA WILAYA YA RORYA MKOA WA MARA MWAKA 2024.**

**A. UTANGULIZI.**

Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga na shule hii kwa mwaka 2024. Ni matumaini yangu utatumia vizuri nafasi hii kwa kusoma kwa bidii, nidhamu na maarifa ili ufaulu vizuri mtihani wa Taifa wa kidato cha nne mwaka 2027.

**B. MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya sekondari Nyamunga ipo umbali wa km 8 toka kibuyi hadi Kinesi. Usafiri wa Basi na bodaboda unapatikana katika kituo cha mabasi Mkengwa na Kinesi. Nauli ni Tshs 1,000/= aidha ununue baiskeli**.**

**C. KUFU NGUA SHULE.**

Shule itafunguliwa tarehe 08 / 01/ 2024 siku hiyo ufike ukiwa na mahitaji yako muhimu shuleni. Muda wa mwanafunzi afikapo aripoti ofisi ya MAKAMU MKUU WA SHULE kwa mapokezi na usajili. Ufike na nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth certificate).

**D. MAMBO YA KUZINGATIA**

**1.1 SARE ZA SHULE**

i. Suruari mbili (2) jani la mgomba iliyokolea na nyeusi mbili (2) zenye marinda mawili zote, mifuko mitatu (mmoja nyumba na miwili yambele ) iwe pana isiyo bana mwili (modo) kwa wavulana.(aje nazo)
ii. Sketi mbili (2) jani la mgomba iliyokolea na nyeusi mbili (2) upana wa marinda ni nchi mbili upana wa makanda usizidi inchi mbili. Sketi iwe ndefu hadi kufunika kisigino (mfano wa sketi umeambatanishwa) kwa wasichana. (aje nazo)
iii. Mashati meupe mawili (2)mikono mifupi kwa wote. (aje nayo)
iv. Tai ndefu mbili (2) moja ya jani la mgomba iliyokolea na moja (1) nyeusi kwa wote. (aje nazo)
v. Soksi nyeupe jozi tatu (3) kwa wasichana na soksi nyeusi jozi tatu d(3) kwa wavulana. (aje nazo)

vi. Viatu vya shule ni vya ngozi rangi nyeusi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi(visiwe na muundo wa BOOT) Kwa wote. (aje navyo)
vii. Sweta moja (1) kijani kibichi lenye alama ya V shingoni kwa wote. (aje nalo)
viii. T – shirt moja (1) yenye nembo ya shule rangi ya blue kwa wote (yenye nembo ya shule na ubora wa hali ya juu inapatikana kwenye duka la shule kwa Tsh 7,000/=)
ix. Sare za michezo ni bukta ya blue na raba kwa wavulana, track suit ya blue kwa wasichana. (aje nazo)

NB: Rangi ya hijabu ifanane na sare za shule.

**1.2 VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI.**

i. Counter book kumi (10) Quire 2 (madaftari makubwa)
ii. Kalamu na penseli)
iii. Mkebe
iv. Rula
v. Four figure

2. **Sheria na kanuni muhimu za shule hii.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini Ofisi ya waziri Mkuu- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Maudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jiioni (Preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali ya umma.

3. **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule kwa mwanafunzi.**

i. Wizi

ii. Uasherati na ushoga.

iii. Ubakaji

iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.

v. Kupigana na kupiga.

vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.

vii. Kudharau bendera ya Taifa.

viii. Kuwa mjazito/kupata mimba.

ix. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

x. Kuoa au kuolewa.

xi. Kukataa adhabu kwa makusudi.

xii. Kuwa na simu ya mkononi.

4. **Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa **MAKAMU MKUU WA SHULE** mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubalina na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

5. **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**ZINGATIA**: Cheti cha kuzaliwa ni lazima mwanafunzi anayekuja kulipoti awe nacho. **Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu zifuatazo:-**

1. **Mkuu wa Shule – 0767 989 595/ 0683 957 084**
2. **Makumu Mkuu wa Shule - 0753-979204**

....................................

**PATRICK M. WADUGU**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NYAMUNGA
S.L.P 1295 MUSOMA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA SHULE**
**YA SEKONDARI NYAMUNGA**
**HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la Ukoo………………………….... Jina la kwanza…………………………………
   Jina la kati ……………………………………………………………………………..
2. Jina la Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………….
3. Kama ni mlezi. Uhusiano ……………………..Namba ya simu…………………………
4. Anwani ya Kudumu ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………..
5. Mahali mwanafunzi alipozaliwa: Mtaa wa/Kijiji cha ………………………………….
   Kata ya ……………………………… Wilaya ya …………………………………….....
   Mkoa wa ……………………………………………………………………………….
6. Dini …………………………………………………… Dhehebu ………………………
7. Unaingia kidato cha ……………………………… Tarehe/Mwaka …………………..
8. Kutoka shule ya Sekondari …………………………………………………………..
   Wilaya …………………………………….. Mkoa …………………………………..
9. Mzazi wako anafanya kazi ya ajira/Mkulima/Biashara ……………………………...
   Mahali…………………………………………………………………………………
10. Usafiri kutoka hapa shuleni hadi nyumbani kwenu ni: (Toa maelezo)
    i. ……………………………………………………………………………………
    ii. …………………………………………………………………………………….
    iii. …………………………………………………………………………………….
11. Ndugu wengine ambao wanaweza kupelekewa habari nzuri juu yako/Maswala ya shule ni:-
    i. ……………………………… uhusiano …………….namba za simu…………...
    ii. ……………………………… uhusiano …………….namba za simu…………...
    iii. ……………………………… uhusiano …………….namba za simu…………...
12. Kabla hujaja hapa shuleni umepimwa na daktari? Ndiyo/Hapana
    Ni ugonjwa upi ni wa kudumu kwako? .........................................................................
13. Sifa maalumu kama unazo/yo ……………………………………………………
14. Unalipiwa/Utalipiwa Karo na: (Taja jina anwani yake na namba za simu)
    ……………………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………………
15. Taarifa za wazazi wako: Wapo…………………………………………………………..
    Wamefariki……………………………………(Weka alama ya vema panapohusika).
    Nakiri kuwa maelezo haliyopo hapo juu ni sahihi.

**SAHIHI YA MWANAFUNZI** **SAHIHI YA MZAZI/MLEZI**

**HATI YA KUKUBALI:** Mimi (Jina la mwanafunzi) ……………………………………………………nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii. Naahidi kufuata sheria zote za shule na taratibu zote kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule

Sahihi ya mwanafunzi ……………………………….. Tarehe …………………………….

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI**:

Mimi Mzazi/Mlezi (Jina)…………………………………………… ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ………………………………………………………. Nimeyasoma masharti ya sheria za shule ya Sekondari Nyamunga ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu za shule. Aidha naahidi kushirikiana na Uongozi wa shule katika malezi bora kwa mwanangu ili baadaye awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

Saini ya Mzazi/Mlezi …………………………………………… Tarehe ………………………

**MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING**
**NYAMUNGA SECONDARI SCHOOL**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**
**(To be filled an Authorized Government Medical Officer)**

Full name(Student)………………………………………………………………. Age …….
Height (In cms)………………………………..Weight (In kgs)………………. ……………

1) Blood count …………………………………(Red and White)………………………
2) Stool Examination ………………………………………………………………..
3) Urine analysis ……………………………………………………………………….
4) Syphilis and other V.D …………………………………………………………..
5) Eye Test ………………………………………………………………………………..
6) T.B and Leprosy Test ……………………………………………………………
7) Ear Test ………………………………………………………………………………..
8) Chest Test ……………………………………………………………………………
9) Abdominal Test ……………………………………………………………………..
10) Blood Group (Very crucial)…………………………………………………………
11) Spleen ………………………………………………………………………………
12) H .I.V Test, Positive ………………………….. Negative……………………………..
(Tick where necessary)

Additional information Eg. Physical defects or impairment, infections, chronic or family Diseases(Eg. Sickle cell)

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

I (Full name)………………………………………certify that the above student is fit/ is not fit pursue Secondary Education

Designation …………………………………

Station ……………………………………….

Signature …………………………………….

Date ……………………………………… Rubber stamp ……………………………………